# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

*MOYO WA MUNGU UKIWA UMEFUNULIWA KATIKA MAISHA YA YUSUFU*

BY JACKIE OESCH

**"NIMEWEKA NENO LAKO NDANI YA MOYO WANGU…"**
**ZABURI 119:11**

Scripture taken from the HOLY BIBLE, NEW INTERNATIONAL VERSION®. Copyright © 1973, 1978, 1984 by International Bible Society. Used by permission of Zondervan. All rights reserved.

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

**Somo 1**

1. **Yusufu na ndozo yake**
2. **Wivu unainuka kati ya ndugu**
3. **Yusufu anauzwa kwa Wamidiani**
4. **Yakobo anadanganywa na wanawe**
5. **Hasira ya baba aliyedanganywa**

**Somo 2**

1. **Yusufu anapelekwa Misri**
2. **Yusufu anaaminika**
3. **Yusufu anajaribiwa**
4. **Yusufu akataa kumtenda dhambi Mungu**
5. **Yusufu anafungwa**

**Somo 3**

1. **Ndoto za wengine**
2. **Yusufu anatafasiri ndoto zao**
3. **Yusufu atafasiri ndoto ya Farao**
4. **Mipango ya Yusufu akiwa Misri**
5. **Yusufu kama kiongozi anafanyia kazi mipango**

**Somo 4**

1. **Wana wa Yakobo wanatumwa Misri**
2. **Dhamira zinawatesa ndugu**
3. **Madai ya Yusufu**
4. **Ndugu wanatumwa nyumbani**
5. **Ndugu waote wanarudi Misri**

**Somo 5**

**Yusufu anakula na ndugu zake**

1. **Ndugu mmoja apendelewa**
2. **Ndugu wanakamatwa**
3. **Ndugu mbele ya Yusufu kwa mara nyingine**
4. **Nafasi ya Yusufu inafabamika**

**Lesson 6**


©2008 FULLVALUE MINISTRIES

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

1. **Ndugu wanaungana tena**
2. **Kurudi nyumbani kwa Yakobo**
3. **Siku ya sherehe**
4. **Msafara wa Yakobo unafika Misrei**
5. **Baba na mwana wanaungana tena**


©2008 FULLVALUE MINISTRIES

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

## UTANGULIZI

Wakati mwingine maisha hayaonekani kuwa mazuri. Tunadhani tunapaswa kulipwa sawa na matendo yetu. Kwamba tukitenda haki tulipwe haki. Tukitenda kwa upendo tunastahili kupendwa. Hatustahili kutendewa vibaya. Tunapanapambana na itikio letu kwa kutotendewa stahili yetu. Tunapotenda vyema kwa haraka tunauliza, "Kwanini haya yanitokee?" Tunaamini kuwa kutenda tukitenda kwa haki tunastahili kulipwa mema.

Sehemu ya kujifunza Biblila iitwayo *Masamaha wa Mungu Uhuru Wetu* ni simulizi inayohusu Yusufu na ndugu zake. Yusufu ni mtoto wa kumi na moja wa Yakobo. Mama yake Raheli alifariki akijifungua mdogo wake na Yakobo aitwaye Benjamini. Yakobo alimpendelea Rahelli kama mke wake na Yusufu kama mtoto wake. Upendeleo huu ulijenga uadui kati ya Yusufu na ndugu zake. Walifanya maisha ya Yusufu kuwa ya shida na siku moja wakaamua kumuondoa. Hawa ndugu walimdanganya baba yao kuwa mtoto wake aliyempenda amefariki. Yakobo alipatwa na majonzi mkubwa kwaajili ya mtoto wake.

Tunajifunza kuwa Mungu alikuwa mwaminifu kwa Yusu pasipokujali shida alizokumbana nazo na kuzuvumilia. Kupitia somo hili tutagundua tutajifunza kuwa Mungu alikuwa pamoja naye akiwa nyumbani kwa ofisa wa Misri , alitenda impasavyo kwa mkuu wa gereza, na alipotenda kwa niaba ya Farao. Hatimaye Mungu alifanikisha kila kitu Yusufu alichofanya.

Ingawa Yusufu alikuwa na hekima na mwenye mafanikio, maisha hayakuwa rahisi. Safari ya maisha yake ilikuwa ya shida. Ilikuwa ni safari ambayo watu wengi wasinge taka kuwa nayo; Pamoja na hiyo hali, hakuwahi kuwa peke yake. Uaminifu wa Mungu kwa Yusufu uliuwa dhahiri kwa wengine. Walifahamu kuwa aliaminika kwa majukumu laiyopewa na kwamba baraka ya Mungu likuwa juu yake.

Tunajifunza kuwa ndugu zake walisumbuliwa na hatia kwa yale waliyofanya. Waliwinda ndugu yao wakitaka kumuua. Hawakujali upendo wa baba yao aliokuwa nao kwa mtoto wake. Hatia hiyo iliwaweka kifungoni na kuwaondolea furaha ya kuishi pamoja kwa amani pamoja na baba yao. Ni nini kingerejesha uhusiano wao na baba yao? Ni kitu gani kingewaweka huru hawa ndugu kutokana ha hatia hiyo?

Habari ya Yusufu na ndugu zake ina uhusiano na maisha yetu. Sawa na Yusufu, na sisi tumeondolewa furaha yetu kuishi na Baba yetu wa mbinguni . Dhambi zimetutenganisha naye. Wote tunafahamu kuwa maisha yetu si matakatifu na hatuishi sawa na Mungu alivyokusudia Matokeo yake tunafanya kwa juudi kumpendeza mzazi sawa na mtoto aliyekutwa na makosa na anafanya juuhudi ya kutenda mema ili arejeshe uhusiano na wazazi wake. Lalini hakuna kilicho chema cha

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

kutosha. Mtoto hafahamu kiasi cha kutosha kinapofanyika kwaajili yake, kuwa amesamehewa kosa na hatia yake.

Je msamaha unatafutwa? Ni vipi mzazi anapotaka tu mtoto akubali kusa lake? Ni vipi mzazi anapotka tu mtoto akiri na kutubu, "Nimetenda dhambi"? Uhusiano unarejea mtotoanaposikia,"Nimekusamehe" Mungu anasikitika kwaajili ya wale waliopotea dhambini na kukakataa zawadi ya upendo na msamaha wake. Siku zote msamaha ni zawadi. Sawa na Yusufu alivyofurahi kuona ndugu zake na kuwasamehe, pia Baba yetu wa mbinguni anafurahi anapoona mmoja wetu akitubu dhambi zake na kupokea maneno ya matumaini kutoka kinywani mwa Mungu, "Nimekusamehe." Tunaishi kwa usalama tukifahamu kuwa Mungu ni mwaminifu na wa haki na anatusamehe dhambi zetu (1 Yohana 1:9).

Simulizi hii ina mwisho wa furaha! Furahia masomo. Kwa mara nyingine angalia *kweli* ya habari hii inavyoeleza juu ya yaliyotokea kwenye familia hii. Jufunze ukweli wa habari kuhusu Mungu hasa jinsi alivyofunua nia yake ya kutusamehe hatia zetu na kutuweka huru toka hatia zetu zote. Kuwa tayari kujifunza juu ya ubinadamu jinsi unavyoona siri za familia hii zinawekwa wazi. Na baada ya kuona ukweli wa simulizi na ukweli juu ya Mungu na ubinadamu, gundua ni kwa vipi habari hizi za zamani zimeandikwa kwaajili yetu sasa, na utafute ni vipi zinafaa katika maisha yetu ya sasa. Zinahusianaje na maisha yangu?

Hebu tuanze! Habari hizi zinaanzia Mwanzo 37 na endelea hadi hitimisho la kitabu cha Mwanzo. Unahimizwa kusoma hizi sura zote. Japo huwezi kusoma habari hizi zote kwa umbali , utagundua kuwa maisha ya Yusufu yanagusa. Karibisha mwingine kushirikiana nao katika kusoma habari hii. Labda hawajasikia habari hii, na mnaweza kukua pamoja katika uhuru ambao Mungu wetu wa mbinguni hutupatia tunapojua kuwa tumesamehewa na kukombolewa, kutoka kwenye aibu na vifungo vyetu vya zamani na mateso ambayo yangetuangamiza. Sherekea uhuru unaopata baada ya kusameh

**KUANZA**

Uanapoendelea na kujifunza Biblia, *Msamha wa Dhambi Uhuru Wertu* utaendelia na safari ambayo itabadilisha maisha yako yaliyobakia. Safari hii itakuwa ya pekee kwako na itategemeana na utayari wako na upendo wako wa kukua katika ufahamu wako juu ya Biblia na kufurahia baadhi ya wahusika wapya kama Yusufu, na ndugu zake. Kujitoa kwako katika masomo kunaleta matumaini ya kuendeleza maisha yako kadiri Mungu anavyoongea nawe kupitia Neno lake.

Unashauriwa kuwa na vifaa vitano mikononi ili kuendeleza uzoefu wako. Vifaa hivi vitatumika kipindi chote cha masomo yako. Utavitumia kila siku ya masomo.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

1. Somo hili la Biblia: *Msamaha wa Mungu Uhuru wetu*
2. Biblia Kumbuka: Kama unakwenda kununua, jitahidi kutafuta Biblia ambayo ina:
    a. Yaliyomo na orodha ya jina la kila kitabu
    b. Kolamu ya rejea amboyo iko chini ya kila ukurasa
    c. Itifaki iliyo nyuma ya Biblia
    d. Ramani za muhimu zilizoko nyuma ya Biblia
3. Kalamu na penseli na kalamu ya kuwekea alama
4. Daftari
5. Kadi ya 3x5 or 4x6

Ukiwaa na viliyoorodheshwa katika #2 utakuwa tayari kujifunza vizuri kwa mafanikio kupitia Biblia. Unaponunua Biblia usisite kumuuliza muuzaji kukusaidia kuchagua, hasa unapochagua Biblia yenye rejea.

Jambo unalopaswa kufahamu: Kuna tafasiri mbalimbali za Biblia.

Usisite kuandika kwenye Biblia yako! Ndiyo maana unakuwa na kalamu, penseli na kalamu ya kupaka rangi. Ifanye Biblia kuwa yako kwa kuiandika ndani, kuipigilia mistari, kuizungushia kuiwekea mishale! Unahimizwa kutumia daftari yako kuandika mawazo, na maswali unapoendelea na safari yako.

Kila moja ya masomo sita limegawanyika katika sehemu tano. Huu mgawanyiko ni kwaajili ya kukusaidia kuendelea na masomo kwa mpango. Kuhusu muda utakaotumia ni juu yako mwenyewe. Wakati mwingine somo linaweza kuhitaji muda zaidi ya muda ulionao jambo ambalo litakufanya umalize somo moja kwa muda zaidi. Wakati mwingine unaweza kumaliza somo moja ukaamua kuendeliea mbele.

Ikiwa ni mara yako ya kwanza kujifunza, unashauriwa kuanza na somo lenye kichwa *Kuifanya Biblia Kuwa Yako*. Ni somo lenye zana zitakazokuwezesha kusafiri katika kujifunza Biblia. *Biblia Kuwa Yako* inaweza kupatikana katika tovuti iitwayo www.FullValue.org. Nakala za ziada ninaweza kupatikana kwa malipo.

- *Mpango wa Mungju Chaguo Letu* ni somo juu ya sura kumi na moja za kwanza za kitabu cha Mwanzo.
- *Ahadi ya Mungu Baraka Yetu* ni habari za Abrahamu inayopatikani katika Mwanzo 12-25. *Uaminifu wa Mungu Tumaini Letu* ni habari za Isaka na Yakobo zilizoandikwa katika Mwanzo 25-36.

Japokuwa somo hili linashauriwa lakini si la muhimu sana katika kufahamu kitabu hiki *Msamaha wa Mungu Uhuru Wetu*.

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Mwisho inakupasa kufahamu kuwa masomo haya yameandikwa ili kukusaidia kujifunza mwenyewe. Yameandaliwa katka hali ya kuwa rafiki yako. Kwa nidhamu fulani utakayojijengea utamaliza masomo haya bila matatizo yoyote, na utafurahaia somo. Utapata taarifa mpya na utahitaji kushirikisha elimu hiyo watu wengine. Na utauliza maswali yenye changamoto yatakayohitaji majibu.

Kwa kutegemea majibu haya unashauriwa kukaribisha wanandoa ambao ni rafiki zako ili kujifunza pamoja nao. Kwa mfano; kuwa katika chumba cha mazoezi ya viungo ni vizuri ukishirikiana na mwenzako. Hii inasaidia kuhimizana katika kuwajibika. Kwaajili hiyo inawezekana wewe na mwenza wako mnahitaji kualika mwanandoa ambao ni marafiki ambao ni majirani zenu. Au mfanyakazi mwenzako sawa na Biblia isemavyo. Au unashirika kweye kanisa ambao lina ukumbi wa kufanyia majadiliano wewe na wanafunzi wenzako katikati mwa juma. Kwa hali yoyote uliyonayo jitahidi kukusanya marafiki mara moja kwa juma ili kujafili pamoja Neno la Mungu. Kila mwana kikundi chenu kiwe kikubwa au kidogo ni wa manufaa kwa kuimarisha wengine! Ni wakati wa kuanza! Fungua Biblia yako katika Mwanzo 37 safari ianzie hapo.

## Somo 1 – Sehemu 1

**UTANGULIZI**: Jukwaa limeadaliwa. Yakobo anaishi katika nchi ya Kanaani, katika mji wa Hebroni, yeye na familia yake. Tulijifunza *Uaminifu wa Mungu Tumaini Letu* kwamba Mungu alimbariki Yakobo kwa utajiri na mali nyingi. Pia alimbariki kwa watoto kumi na wawili ambao aliwapata kwa wake zake Lea na Raheri pamoja na vijakazi vyao.

Tunapoendelea na habari za Yakobo tutajikita zaidi kwa Yusufu. Tunachagua habari iliyo katika Mwanzo 37. Yusufu ni kijana mdogo, ana umri wa miaka 17, mchungani anayechunga mifugo na kaka zake. Chukua muda wa kukumbuka maisha yako ya umri wa miaka 17. Kwanye daftari yako andika majibu ya maswali yafuatayo: Mambo gani yalikuwa yakiendelea katika umri huo? Ulikuwa na hekima gani? Ulikosa mambo gani kipindi hicho? Kama wewe ni mdogo zaidi fikiria kuwa na umri wa miaka 17. Ungetaka uweje utakapofikia miaka 17?

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mwanzo 37:1-11.

**ZOEZI**:

- Tunaambiwa nini katka mwisho wa mstari wa 2 kwamba Yusufu analeta kwa baba yake?

  ______________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Tuna majina ya wahusika wanaosemwa! Ni aki na nani? ______________________

- Mstari 3 unatusaidia kufahamu mahusiano ambayo yamekuwapo kwa siku nyingi.

  Tunaambiwa nini? ____________________________________________________

  Yakobo amefanya nini mpaka akaonyesha upendeleo wake?

  __________________________________

- Mstari wa 4 ndugu zake Yusufu wanafanyanini kufuatana na upendeleo wa baba yao wa wazi?

  ____________________________________________________

**FUNDISHO**: Jamani , unaona mahangahiko? Upendeleo wa wazi wa Yakobo kwa Yusufu unajenga hasira kwa kwa kaka zake kufuatana na kuwasema kwake kwa baba yao. Chuki yao inaanza kula fikra zao. Hawasemi jema lolote kwa Yusufu. Je tunaweza kushangaa Yakobo kuwa na mtoto mwenye upendeleo? Kumbuka mazingira ambamo Yakobo alilelewa (Mwanzo 25:28). Mwanzo 29:30 inatuambia kuwa alimpenda Raheli kuliko Lea. Upendeleo unavyozidi kupenya unaingilia nyumba ya Yakobo, na chuki kati ya watoto wake wakubwa kwa mdogo wao inaongezeka.

**ZOEZI**: Yusufu anaota (Mwanzo 37:5).

- Ndugu zake waliitikiaje baada ya kuwashirikisha ndaoto yake katika mstari wa 5?

  ____________________________________________________

- Ndoto yake ilihusu nini (mstari 7) kwa maneno yako?

  ____________________________________________________

- Kaka zake walimuuliza. "Je unamaana kuwa _____________sisi? " Kwao ndoto ina maana hiyo.
- Hatuwezi kupuuzia hii kwa mara ya tatu katika mistari hii tunaambiwa kwamba hawa ndungu waliambiwa kwamba _______________. Ndoto yake na aliyoyasema yaliwakasirisha. Pigilia mstari maneno chuki aliyotajwa mara tatu.
- Mara nyingine mtu hawezi kusaidia bali kushangaa. Kulitokea nin katika mstari 9?

  ____________________________________________________

- Wakati huu ni ndoto gani? ____________________________________________________
- Yakobo aliitikiaje kuhusu ndoto hii?

____________________________________________

- Mstari wa 11 itikio la ndugu zake nini juu ya ndoto hii? _____________________
  Itikio la baba yake lilikuwa nini? _________________________________________
- Upendelio ulizaa chuki ilichochewa na wivu wao. Baba yao alitafakari tatizo katika mawazo yake. "Baba yao *alimpenda* yeye zaidi." Chuki yao na wivu vilijengwa katika upendeleo wa baba yao. Alimpenda Yusufu kuliko ndugu zake wengine… (Mwanzo 37:4)

**Somo 1 –Sehemu 2**

**FUNDISHO**: Wivu siyo neno jipya. Kama ujuavyo Raheli alikuwa na wivu kwa dada yake Lea kutokana na kupata uzao wakati yeye alikuwa tasa. Wivu unaonyesha picha ya ukatili na hofu, hakuna dalili ya uungu. Hali haionyeshi sifa ya Mungu ya upendo na huruma bali hali ya mtu kupewe asichostahili. Ni moto unaounguza ndani ya mtu kumiliki cha watu wengine. Katika somo la 5 – Sehemu ya somo liitwalo *Uaminifu wa Mungu Tumaini Lwtu* weivu kati ya Raheri na Lea umejadiliwa. Hali ya dhambi iliyoonyeshwa na hawa ndugu imeathiri mahusiano ya hawa ndugu.

**KUCHIMBA KWA KINA**: Mwanzo 37:11 inasema, "Ndugu zake walimuonea wivu." Andika rejea mbili ambazo zinaweza kuwa zimeonyeshwa katika Biblia yako.
Angalia katika Matendo Acts 7:9. Rejea ya Agano Jipya inatwambia nini kuhusu yatakayotokea baadae? Wivu wao unawaongoza kufanya nini?

__________________________________________________

**ZOEZI**: Rundi Mwanzo 37.

- Mstari 12: Ndugu walikwenda wapi? ____________________ Walikuwa wakifanya nini huko? ______________________________________________
  Tafuta Shekemu kwenye ramani nyuma ya Biblia. Onyesha Shekemu Kaskazini mwa Yerusalemu na Kaskazini mwa Betheli. Unafikiri ni umbali gani kati ya Hebroni na Shekemu? ____________
- Mstari wa 13: Israeli (Yakobo) alimwambia nini Yusufu?
  ____________________________________
- Mstari 14: Maeliekezo ya Yusufu yalikuwa nini?
  _____________________________________
  Kumbuka yaliyotokea Yusufu alipokuja na taarifa(mstari 2)?
  ________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

- Yusufu alikuwa na mwendo mrefu wa kusafiri. Alipofika huko alipata wakati mgumu wa kuwapata kaka zake. Anagundua nini katika mistari ya 15-17?

  ___________________________________

  Dothan ni karibu ya maili 10-15 kaskazini mashariki. Kwa gari mwendo huu hauonekani kuwa mbali lakini tukikumbuka Yusufu akisafiri kwa miguu kupitia njia mbovu zenye myamba za Kanaani tunapata picha tofauti ya safari ya Yusufu.
- Aliwapata ndugu zake Dothani, lakini mstari wa 18 unatwambia nini? ____________________________________________________Chuki yao ilikuwa imekua kiasi cha kuamua kumuua ndugu yao. Labda hatuwezi kushangaa kwasababu katika Mwanzo tunasoma kuwa chuki ya Kaini ilimfanya kumuua ndugu yake Kaini.
- Ndugu walipomuona walisema nini? _________________________
- Walipanga kufanya nini katika mstari wa 20?

  _____________________________________________

  Walipanga kusema nini? __________________________________________

  Inaonekana ndoto ya Yusufu ilikuwa shida ya mwisho. Hawa ndugu waliisha kuwa na chuki za kutosha! Waliamua kumuonyeha ni kipi kinacho tokea baada ya ndoto yake.
- Ni ndugu yupi aliyejaribu kumuokoa? ____________________Tunajifunza nini kuhusu yeye katika Mwanzo 29:32? ____________________________________________________
- Rubebi alitoa mpango gani mbadala? ______________________________________

  Alikusudia kufanya nini? ____________________________________________________
- Katika mistari ya 23-24 ndugu walifanya kile walichopanga. Walimvua nguo yake nzuri aliyokuwa amevaa kumtupa shimoni jangwani. Shimo lilikuwa halina majiWhile they were eating, waliona nini katika mstari wa 25? ________________________________

  Msafara wa Waishmaili walikuja. Tumia mistari ya rejea kuona waishmaili walikuwa aki nani.

  ____________________________________________________

### Somo 1 –Sehemu 3

**ZOEZI**: Waishmaeli walikuwa wakito Gileadi. Kuonyesha Gileadi katika ramani yako tazama jimbo sio mji. Kama ramaini yako haionyeshi Gileadi iko magharibi mwa mto Yordan. Sehemu ya kaskazini inafika bahari ya Galilaya (au bahari ya Chinerasi) na sehemu ya kusini ilizogea chini kuelekea kona na bahari ya chumvi. Masafara ulikuwa ukitoka Gilead ukienda Misri. Walikuwa wamebeba nini? _________________________________________________________

- Yuda alipendekeza nini kwa ndugu zake mistari 26-27?

  ____________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Ndugu wengine waliitikiaje? ____________________________________________

- Katika hatua hii tunahitaji kurudia baadhi ya mambo ili kukumbusha fikra zetu:

  Waishmaili: ukoo wa mwana wa Ibrahimu Ishmaeli (Mwanzo 16:16)

  Wamidiani: uzao wa Abraham na mke wake Ketura (Mwanzo 25:1-4)

  1. Wamidiani: Nchi kusini ya mbali kusini mwa bahari ya chumvi.
  2. Msafara huu wa Waishmaeli yamkini ulianzia katika nchi ha Wamidiani, kwahiyo pia wangeitwa Wamidiani. Walisafiri kaskazini mwa Geliradi na kukatisha Kanaani ambako ndugu waliwaona wakikaribia mji wa Dothan.

Kumbuka: Haya maneno si lazima katika kujifunza kuyazoez kutafanya Biblia kuwa nyepesi. Labda unajifunza sehemu ya ulimwengu wa zamani na mila zake ambazo ulikuwa hujajifunza kabla. Endelea kutembea! Unafanya vizuri!

- Wafanyabiashara wa Kimidiani walikuja Ndugu walifanya nini?

  __________________________________________________

  Wafanya biashara walimchukua Yusufu wakaenda naye Misri.

- Baadae ni nani aliyepoteza mwelekeo na maendeleo? _________________
- Msaada wa Rubeni ulishindwa. Kisima hanina maji. Yusufu amekwenda! Yuko katika hasara ya afanye nini. Anasemaje (mstari wa 30)? _________________________________
- Sasa kifuniko kikubwa... Katka mstari wa 31 Ndugu wanafanya nini?

  __________________________________________________Wanamwambia nini baba yao 32?

  __________________________________________________

### Somoo 1 – Sehemu 4

**FUNDISHO**: Hii siyo habari ya kwanza ya kifuniko katika Biblia Je unakumbuka ya kwanza Mwanzo 3:7. Tunapofanya jambo baya jambo la haraka la kufanya ni kujifunika na kujificha. Adamu na Eva walishona majani ya miti kujifunika na kujificha vichakani. Hakukuwa na njia nyingine ya hawa ndugu ya kuangalia waliyoyafanya. Mpango wao wa kumuua Yusufu ulishindwa. Walikuwa ni watumwa wa hila zao mbovu. Wamechukua nguo ya yuke, wakaichovyo damuni na kumpelekea baba yao. Baba yao alipokea nguo ya mtoto wake aliyempenda sana iliyojaa damu na kuamini kuwa amekufa.

**KUTAFAKARI**: Ingekuaje kwako kupanga njama za kumuua ndugu yako? Inaweza kuwa ni jambo baya kiasi gani kiasi cha kupanga kuua mtu? Inaonekana hawa ndugu walikuwa na wivu ukiwaka ndani yao kwa miaka 17 ya umri wa Yusufu. Dhambi hujenga chuki na kukua ndani ya maisha ya

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

mtu pasipokuipima huishia na mauti. Kumbuka mtume Paulo alichosema katika Wagalatia 5:19-21. Ni matendo gani ya dhambi anayoorodhesha Paulo?

___________________________________________________

Paulo anaonya nini kuhusu matendo haya? _______________________________

- Methari 16:25 inatwambia kuwa kile kinachoonekana kuwa kizuri kinaweza kutuelekeza kwenye ______________.
- Katika Warumi 8:10-14 inaongelea kuhusu Kristo kukaa ndani yako na wajibu ulionao. Mstari wa 13 unasema kuwa tukiishi katika maisha ya dhambi kutatokea nini?

  ____________________

  Lakini tukiishi katika Roho…tuna__________________________________.

**KUKARIRI**: Warumi 8:10-14 ina nguvu.

- Soma msitari hii kwa makini na ujaribu kutafakari upendo wa Mungu kwako. Anakutakia maisha ya miele!
- Andika mstari 13 na 14 katika kadi.
- Unapokariri mistari hii juma hili kumbuka maswali haya ya matumizi:
  - Ni sehemu gani katika maisha yangu ninajikuta nikishi maisha ya dhambi (Wagalatia 5:19-21)?
  - Ni maeneo yapi katika maisha yangu ninayofahamu kuwa Mungu anafanya kazi ndani yangu na kuniwezesha kuishi kwa kuongozwa na Roho wake (Wagalatia 5:22, 23)?
- Andika majibu ya mswali haya nyuma ya kadi. Tunza kadi hizi mikononi kwa kukariri na kuandika notisi juma hili lote.

**Somo 1 – Sehemu 5**

**MATUMIZI BINAFSI**:

- Ni ndugu wapi unaweza kukumbuka ? Reubeni, Yuda au mmoja wa wanane. Je ungekuwa kati ya ndugu wanaokubalika (mstari 27)? Kwanini ndiyo au hapana

  ______________________________________________

  Ungekuwa upande wa upinzani ukifahamu kuwa ni vizuri? Ni mambo gani lingekufanya uwe hivyo?
  Ungekuwa wakili wa Yusufu? Pamoja na yote yaliyotokea ungesemaje kwa ndugu zake?

  _______________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

- Reuben alikuwa mtoto mkubwa na kwa hali hiyo aliwajibika kwa wadogo zake. Je uliisha pewa wajibu kwaajili ya mtu mwingine na badala yake ukajiangusha nafsi yako na watu wengine pia? Hali hiyo ilikuwaje kwako?

  ___________________________________________________

  _____________________________________________________

- Je unaweza kujifananisha na Yuda? Yuda alitaka Yusufu aondoke lakini hakutaka kumuua. Aliwaambia ndugu zake kuwa wasingepata faida yoyote kama damu ya ndugu zao ingekuwa mikononi mwao. Je ungeweza kupingana na ndugu hawa wenye hasira? Ungewaza kufanya nini zaidi? _____________________________________________________

- Ni tabia gani mtu anapaswa kuwa nayo ili kuwa kinyumbe na hali hii ya dhambi ya wivu ambayo matokeo yake yanasababisha mauaji?

  _____________________________________________________

- Ni wakati gani katika maisha yangu ambapo wivu ulivuruga maisha yangu kiasi cha kulitawala maamjuzi yangu?

  _____________________________________________________ Badala ya kuwatia moyo wengine na kuwasaidia kwa upendo na kujali mahitaji yao, ni mambo gani huchugua kufanya? Kwa mfano: Je ninashiriki katika maongezi kwa kutumia maneno yawezayo kuleta uaharibifu? Je hupindisha ukweli na kuunga mkono uongo? Je huruhusu nafsi yangu kulinda waarifu? Huchagua kufanya mambo gani?

  _____________________________________________________

**SALA**: Bwana Mungu, mara nyingi huwaza hali yangu ya wivu. Ninaonea wivu nafasi za wengine, upendo wa wengine, Urafiki na mahusiano ya wengine. Niaona wivu kwaajili ya karama, uwezo, na ufahamu wa wengine. Ninatamani kuridhika na hali yangu niliyo nayo na kuachana na mawazo mabaya. Ninajiona kuwa siko tofauti na ndugu zake na Yusufu. Nisamehe Bwana Yesu. Siwezi kufanya badiliko lolote nipendalo maishani mwangu kwa uwezo wangu. Nina kutegemea wewe kabisa kuniwezesha kwa Roho wako Mtakatifu, kuniongoza, na kuniwezesha kuishi kwa uhuru na mwana wa Baba wa mbinguni aliyesamehewa. Ninaomba kipekee msaada katika eneo hili la maisha yangu. ___________________________________________________________
Asante kwa kuniondolea hatia niliyobeba siku nyingi. Uhuru wako unaniwezesha ku___________________________________________

**FUNDISHO:** Baba yao aliumia moyoni. Alitmbua vazi. Alihisi kuwa mtoto wake ameliwa na wanyama wakali. Uchungu wake ulimfanya ararue mavazi yake na kulala kwenye mjivu akiomboleza.

Wana na mabinti zake walikusanyaika lakini hakukubali farafa yao. Aliomboleza akisema kuwa angekwenda kaburini akimuombolezea mtoto wake. (Mwanzo 37:33-35)

Inawezekana kuwa kuna matukio kuvumilia kufuatana na mambo mabaya tuliyowafanyia wengjne. Tunapaswa kufahamu kuwa Mungu ni mwaminifu na hatatuacha hata wakati wa shida. Silaha za upendo wa Mungu wetu wa mbinguni hutulinda. Hata sisi tunaweza kuwalinda wenzetu wanaoteswa na matukio waliyoyafanya zamani.

Yakobo alikuwa mdanganyaji. Alikulia katika nyumba ya kudanganya. Alimdanganya baba yake na kaka yake. Aliishi kwa kukimbi kaka yake. Alidanganywa na mjomba wake kwa kupewa mke tofauti na makubaliano yao. Sasa watoto wake mwenyewe wamemdanganya. Wivu, na uongo, zote ni kazi za mwovu. Pamoja na tabia nyingi zilinazoonekana katika familia hii, bado Mungu anapitisha upendo wake kwao. Kadiri habari ya Yusufu inavyoendelea tutamuona Mungu kama mshindi.

### Somo 2 – Sehemu 1

**UTANGULIZI**: Tayati katika Mwanzo 37 tumejifunza kuwa kiburi, uongo, na mawazo ya mauaji yameingilia nyumba ya Yakobo. Baba anaachwa amebeba vazi la mtoto wake mpendwa likiwa limejaa damu, akiomboleza bila faraja, akiamini kuwa Yusufu ameuawa na wanyama wakali. Kwa makusudi ndugu wamemumuuza mdogo wao mwenye kujidai na sasa wametafuta jinsi ya kuficha huo uovu wao. Japo wameuza mdogo wao kwa Wamidiani wafanya bishara wa Misri, lakini baba yao anaamini kuwa mtoto wake amekufa.

Nini kilitokea kwa Yusufu? Tuache Yakobo na watoto wake twende Mwanzo 39. Mwanzo 37:36 inatwabia kuwa, wakati huo huo, msiba ukiendelea nyumbani mwa kwa Yakobo, Wamidiani walimpeleka Yusufu Misri na kumuuza kwa Potifa ofisa mmoja wa Farao, na ofisa wa jedshi.

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mwanzo 39:1-6. Mstari 1 karibu ni marudio ya 37:36.

**ZOEZI**:

- Ni mambo gani ya kwanza tuliyojifunza katika mstari 2?
    1. ______________________________
    2. ______________________________
    3. ______________________________
- Ni mambo gani yaliyompata Potifa mpaka akampa upendeleo Yusufu (mstari 3)?

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

1. ______________________________________________
2. ______________________________________________

- Yusufu alikuwa na wajibu gani akiwa muudumu nyumbani kwa Potifa (mstari 4)?
    1. ______________________________________________
    2. ______________________________________________
- Mmisri na watu wote wa nyumba yake walibarikiwa kutokana na Yusufu (mstari 5). Katika mistari ya 2-5 pigia mistari au upake rangi mistri na maneno yote inayotaja Bwana. Tunajifunza nini juu ya mistari hii kuhusiana na matokeo ya baraka za Mungu kwa watu wake, na matokeo yake.Hizi zinakwenda kwa watu wengine?

    ___________________________________________________

- Mwisho wa mstari wa 5 unatwambia

    ___________________________________________________Kwasababu Mungu alikuwa akibariki kila jambo, wajibu wa Yusufu ulikuwa ni nini? Potifa alimpa wajibu gani?

    ______________________________________________

- Potifa alihusika na kitu gani tu (mstari 6)? _________________________________

### Somo 2 – Sehemju 2

**MATUMIZI BINAFSI**: Watu wa Mungu huishi chini ya baraka zake . Pamoja na hayo Mungu hubariki watu wengine kupitia watu wake.

- Mungu alisema nini kwa Abram katika Mwanzo 12:2-3?

    ___________________________________________________

- Mungu alimwambia Abrahamu kuwa atakuwa Baraka na atawabariki wote watakaombariki…na kwamba watu wote wa dunia watabarikiwa kupitia yeye. Kumbuka mahusiano ya habari hii na maisha yako:
    - Ni aki na nani wanaoishi katika uwezo au miliki yako, mfano,majirani, wafanyakazi wenzako, marafiki? Taja majina maalumu. ______________________________
    - Kumbuka wanavyobarikiwa na Mungu kupitia wewe, mfano usalama na ulinzi, ukweli, ulinzi, tabia njema na kujiamini?

        ______________________________________________

**KUKUMBUKA** Kwa faida yetu na watu wengine tunapaswa kulishika Neno la Mungu. Tunavyoendelea kujifunza tunazidi kufahamu Yeye ni nani na ni vipi anataka tubarikiwe na kuwabariki wengine kupitia sisi. Kazi ya kufanya kuhusu kumbukumbu ni Zab. 1:1-3.

- Katika mstari 1 ni mazingira yapi matatu tunapaswa kuepuka?
    1. ______________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

2. ___________________________________________
3. ___________________________________________

- Ni jambo gani mwandishi wa Zaburi anatuambia kufuarahisa kaftika mstari wa 2?
  1. ___________________________________________
  2. ___________________________________________
- Mwisho ni mifano gani imetolewa katika mstari wa 3?

  ________________________________

- Elezea mti. Umepandwa wapi? Hali yake ikoje?

  _______________________________________________

- Tukiwa watu wa Mungu waliobarikiwa, ni watu gani wanaobarikiwa na Mungi kupitia sisi? Njia nyingine ni kuuliza swali: Ni aki na nani waliojenga viota vyao mbavuni mwangu na kupata kimbilio na usalama kwenye matawi yangu?

  _______________________________________________

Andika maneno haya kwenye kadi na furahia fursa ya Mungu kukuonyesha njia ya kuwa mti mkubwa, wenye nguvu na wenye uhai, mti utoa kivuli kwa waliochoka; mti utoao matawi yenye usalama ambako wengine hupata pumziko lao. Andika uzoefu wako nyuma ya kadi. Mshukuru Mungu kwa kukuchagua kuwa njia ya kubariki watu wengine.

**SALA**: Bwana Mungu ulimbariki Potifa na nyumba yake kupitika Yusufu. Ulibariki vyote alivyomiliki, vyote vya shambani na nyumbani. Yusufu alileta uwepo wa upendo wako nyumbani kwa Potifa. Nifumbue macho yangu nione unavyonibariki na kupitia mimi vinavyobarikiwa. Unawabariki hata wale wasiokufahamu. Naomba maisha yangu yawe kwaajili ya makusudi, ya kubariki watu wengine, sawa na ulivyonibariki mimi kwa uaminifu wako. Watu wengine wakufahamu wewe ninayekuomba. Wakufahamu na kupataa baraka zako

_____________________________________________________

**Somo 2 – Sehemu 3**

**UTANGULIZI**: Kwasababu tu tuko katika uhusiano na Mungu katika imani yetu kwa Yesu si kwamba hatukutani na maovu katika ulimwengu wetu. Unaweza kukumbuka toka masomo yaliyopita ya Mwanzo 3 katika *Mpango wa Mungu Chaguo Letu* vita na hasira ya mwovu inatufuatilia. Mistari sita ya kwanza ya Mwanzo 39 intuambia habari njema ya barika ya Yusufu sasa maisha yake yaliyobaki yanafuata. Swali linabaki: Je Baraka ni yale mambo mema tu? Mungu anabarikije huyu mtu wa imni wakati anishi kwenye mazingira magumu ? Ni lini Mungu anaweza kutumia mazingira yale kuwa baraka? ___________________________

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mwanzo 39:6b-23.

**ZOEZI**:

- Yusufu anaelezewaje katika mstari wa 6b?

  ______________________________________________

- Ni maneno gani yanaayofuata katika mstari wa 7? Ni majaribu gani yanayoletwa na mke wa Potifa?

  ______________________________________________________Mke wa Potifa anavutiwa na mwonekano wa nje wa Yusufu na anakuwa mjaribu.

- Mstari wa 8: Yusufu anamkataa. Andika majibu yake. Kwa umakini kumbuka maneno yake: ______________________________________________________Alikuwa akiwajibika kwa nani? _____________________________________________________

  Bwna wake Yusufu alimwamini Yusufu katika mambo ya nyumba yake yote, na hakujihusisha na kitu chochote nyumbani kwake. Yusufu alikuwa jemadari wa pili. Bwana wake hakumnyima kitu chochote isipokuwa mke wake. Anauliza swali katika mwisho wa mstari wa 9: ___________________

  ______________________________________________________

- Yusufu alikuwa kijana mwenye afya. Alikuwa akijaribiwa sawa na wanaume wengine. Mke wa Potifa alifahamu hali hiyo na kwasababu hiyo alikuwa akimwalika mara kwa mara. Biblia inasema nini kuhusu Yusufu katka mstari wa 10?

  _________________________________________________

- Kwanini eneo hili linaongelea habari za mke wa Potifa?

  ___________________________________

**KUCHIMBA KWA KINA:** Hebu tuangalie sehemu nyingine za Biblia inayoelezea wanawake wanaojaribu wanaume kufanya nao ngono. Mafalme Sulemani aliandika mengi katika kitabu cha Methali kwaajili ya mwana wake. Katika Methali 6 na 7 Sulemani anamuangaliza mwana wake kuhusiana na zinaa. Unaweza kusoma hiki kifungu chote lakini kwaajili ya kujifunza hebu tushirikishane hekima ya Sulemani ya kumlinda mtoto wake na zinaa, kutokana na kukutana na wanawake wasio na maadili, na malaya. Kwa makini soma Methali 6:20-35. Fikiria mazingira ambamo Yusufu alijikuta.

- Yale Sulemani anayomwambia mtoto wake ni makusudi, au mafundisho (mstari 23)?

  ______________________________________________________

- Katika mstari wa 24 anasema kuwa mafundisho haya yatalinda mtoto wake kutoka wapi?


©2008 FULLVALUE MINISTRIES

____________________________________________Mstari 26: Sulemani anasema nini juu ya mwanamke malaya na mzinzi?

____________________________________________

- Mstari 29-35: Ni matokeo gani yanayotokana na mtu anayelala na mke wa mtu mwingine?

  ____________________________________________

Sulemani yuko wazi kwa mtoto wake. Hekima yake ya ukweli inatufundisha sisi pia. Tunapaswa kuyaweka mioyoni mwetu siku zote kwasababu yatatuongoza, angalia, na utwambie.

### Somo 2 – Sehemu 4

**ZOEZI**: Fungua tena Mwanzo 39:11.

- Ilitokea nini Yusufu alipokwenda kufanya shughuli zake za kawaida?

  _________________

  ____________________________________________

  Kwa kudhamiria alimuamuru Yusufu alale naye. Yusufu alimkimbia na katika kufanya hivyo aliacha _____________ mikononi mwake (mstari 12) ambacho kilikuwa kielelezo cha mke wa Potifa kutengeneza uongo wake. Tamaa yake ya zinaa na madaraka vilimfanya amdharirishe Yusufu kwasababu ya kumkataa na kukimbia. Alibuni maneno ambayo yangemuumiza Yusufu. Hadithi yake ilikuwa nini katika mistari ya 3-18?

  ____________________________________________

  Katika mstari wa 19 alimwambia nini Potifa aliporudi nyumabani?

  ______________________

  ____________________________________________Aliitikiaje?

  ______________unashangaa (Mithali 6:34)?

- Potifa alimfnyia nini Yusufu (mstari 20)? ________________________________

**KUTAFAKARI**: Mistari ya kwanza ya Mwanzo 39 inatuambia jinsi kijana Yusufu alivyoheshimiwa. Alikuwa mwenye sura ya kuvutia, aliyetegemewa, na mwaminifu, Alikataa hata kulala na mke wa bwana wake pasipokujali ni kwa kiasi gani ingemgharimu. Sasa Yusufu anatendewa kama muhalifu. Anatupwa magerezani na mtu aliye mwamini kabisa, mtu aiyemtambua Yusufu kama mtu liyebarikiwa na Bwana. Haya yote yalitokana na uongo wa mke wake Potifa. Tunaambiwa kuwa Potifa "alipandwa na hasira." Yusufu amezuiliwa mahali ambapo wafungungwa wa bwana wake wanawekwa, mahali ambapo si pa kujichagulia.

Kwanini Yusufu? Kijana mzuri kama huyo… Kwanini yeye? Mungu alikuwa wapi? Mungu alikuwa naye tu akiwa nyumabani kwa bwana wake na mazingira ya utajiri na maarufu? Ni kwanini Mungu

aruhusu mambo mabaya yampate mtu mwema kama huyo? Unaweza kusema kuwa kama ndiyo njia Mungu afanyavyo basi nina jambo la kujadiliana naye.

Fikiri kuwa wewe ni Yusufu. Ni wewe uliye kwenye gereza lenye giza , na wafungwa wa mfalme. Ni maswali gani yanaweza kuwa yanaendelea katika mawazo yako? Ni jambo gani unaweza kuwa unamlilia Mungu wako? Maisha ambayo yalisababishwa na ndugu zako ulikuwa hujawa mbaya, lakini sasa!

______________________________________________________

**KUCHIMBA KWA KINA**: Tunachukia uonevu. Tunakuwa na uchungu kwa wale wanaotuonea. Katika 1 Petro 2:21-25 tunaitwa kwa wito mkubwa. Angalia mistari hii ambayo Petro anafanya rejea kwa Yesu ambaye ni mfano wetu wa.

- Petro anasema kuwa tumeitwa kuwa kama Yesu. Yeye_____________________ na akatuacha kama ________________________ ili tuweze _____________________ katika nyayo zake (mstari 21).
- Petro ananukuu Isaya 53:9. Yesu hakutenda dhambi (mstari 22). Tunaambiawa kuwa alifanya nini alipodhiakiwa wakati wa mateso yake? ______________________________

  ________________________________________________
- Mstari 23 unaendeliea kusema kuwa Ali

  _____________________________________________

  Hiyo ina maans gani?! Yesu alikuwa amebeba mapenzi ya Baba yake. Yesu alijikabidhi kwa baba Ambaye alifahamu kuwa ni wa haki na kweli katika hukumu yake.
- Yesu alikuwa tayari kubeba dhambi zetu mwilini mwake msalabani ili ____________ ____________ _____________ ______________________. Mimi na wewe tumepona kutokana na kazi aliyotufanyia Sisi ni kama ________________ aliyepotea na sasa ame ________

  (mstari 25).

**Somo 2 – Sehemu 5**

**ZOEZI**: Turudi kwa Mwanzo 39 tunaona kuwa sura inamalizika na Yusufu akiwa gerezani.

- Kwa mara nyingine, katika mstari wa 21 tunasoma maneno matano ambayo karibu yanafanana na mstari wa 2. Mstari huu unasemaje?

  ________________________________________________
- Mstari unaendelea kuonyesha jinsi Mungu alivyojidhihirisha kwa Yusufu akiwa gerezani.

  ________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

- Katika mstari wa 23 tuanatambua kuwa mwenendo wa Yusu ulitambuliwa na mwangalizi wa magereza. Alitoa wajibu gani kwa Yusufu?

  ______________________________________

- Mtunza gaereza alitapa nafuu alipompata Yusufu kama msaidizi wake. Mstari 23 unatwambia kuwa msimamizi wa magereza

  ______________________________________________

  Alifahamu kuwa Bwana alikuwa naye na kumfanikisha katika mambo yote aliyofanya.

- Angalia hali ya kufanana kati ya Potifa aliyoyaona kuhusu (mstari 3) na msimamizi wa gereza (mstari 23). ___________________________________________
- Potifa (mstari 5) na msimamizi (mstari 22)waliweka Yusufu kuwa msdimamizi wa yote waliyokuwa wakiyafanya. _____________________________________________

**KUTAFAKARI**: Mtu hawezi kusaidia zaidi ya kushangaa kile Yusufu alichofanya kiasi cha kukubalika machoni mwa msimamizi wa magereza. Yeye kama mfungwa ni kitu gani anachoweza kuwa amefanya cha kuvutia. Yusufu amekuwa muhanga wa uongo na ametendewa isivyo haki. Amefungwa na bwana wake wa zamani, akiwa amejaa hasira. Yusufu hakufahamu ni kwa muda gani angeishi humo labda maisha yake yote. Hatupaswi kufahamu kuwa alikuwa mgeni nchini. Mila na desturi za Misri zilikuwa tofauti na za kwa baba yake ya kuchunga wanyama na maisha ya kuhamahama. Misri ilikuwa kama nchi iliyostaarabika na yenye maendeleo na jamii ya walio elimika. Farao alikuwa kiongozi wa Misri, kilio kutoka kwa baba yake aliyekuwa karibu naye akiwa amemzoea. Ineakuwa umefungwa pamoja naye, unafikiri uzoefu wako ungekuwa ni upi ambao ungekuwezesha kuwaambia wengine kuwa Mungu alikuwa pamoja naye

___________________________________________________**MATUMIZI BINAFSI**:

Fungua 1 Petro 3: Yusufu ni mfano wetu wa kufuata. Kwa vyoyote alikuwa mtu wa Mungju aliyevutia wengi. Na kipekee tunaona kuwa alivutia macho ya waliokuwa kwenye madaraka juu yake. Mstari wa 9 inaonekana kuwa ni jinsi alivyoishi tangu alipouzwa na ndugu zake kwenda Misri. Andika mstari huu kwenye daftari yako.

___________________________________________________Yusufu aliona kuwa ameitwa kuwabariki wengine. Matendo yake kwa wengine hayakutegemea alivyotendewa yeye. Alikabidhi maisha yake kwa Yeye ahukumuye kwa haki (1 Petro 2:23). Mistari hii juu ya maisha ya Yusufu imekupa changamoto gani? ___________________________________________________

Ni kwa namna gani mwenendo wako, uchaguzi wako wa maneno ya kusema, matendo yako huleta mabadiliko katka maisha ya wengine?

___________________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Hii inaleta changamoto gani kwako unapokumbuka kuwa umebarikiwa na Mungu ili kuwa Baraka kwaajili ya wengine? ______________________________________________

**SALA**: Bwana, Nataka kuwa kama Yusufu. Nataka kuleta tofauti katka maisha ya wengine. Nataka nijaze dunia na upendo wako ili huruma yako iweze kuvuta wengine kwako. Niepushe na uchungu na kukata tamaa wakati wa matatizo. Nisaidie kuwasema vizuri walio katika madaraka juu yangu ili niweze kuwaonyesha upendo wako.

______________________________________________

**Somo 3 – Sehemu 1**

**UTANGULIZI**: Tuliishia somo la 2 kwa uonevu Yusufu akitupwa gerezani kutokana na ongo wa mke wa Potifa. Alikuwa na nafasi ya heshima akiaminiwa na bwana wake kwa kila kitu kilichokuwa nyumbani mwake. Alikataa kujaribiwa kwa mara kwa mara kwa mke wa bwana wake ili alale naye akakimbia na kumwachia nguo yake. Mke wa Potifa alidangnya, mme wake akamwamini. Yufufu anajikuta gerezani pasipo na dalili ya matumaini ya kuonyesha kuwa atatoka.
Pamoja na hayo yote yaliyompata tunajifunza kuwa Mungu alikuwa pamoja naye gerezani, Anamfanyia ukarimu na kumpa kibali mbele ya mwangalizi wa gereza ambaye alimfanya awe kiongozi wa wafungwa wenzake. Aliaminiwa kwa kila kitu kilichokuwa kule. Mwangalizi wa gereza alijjua kuwa Bwana alikuwa na Yusufu kwasababu kila alichokifanya kilifanikiwa.

Kuwa kiongozi na kufanikiwa kilileta tofauti gani wakati yuko magerezani? Kama Mungu alikuwa naye asingemtoa gerezani?

**KAZI YA KUFANYA**: Habari inajirudia katika Mwanzo 40 na 41. Kwasababu ya sehemu ya somo hili liyobaki hatutaweza kujifunza masomo yote kwa upana wake Maswali ya mazoezi yatakusaidia kukupitisha katika somo hili. Unashauriwa kusoma, kujifunza, na kuuliza maswali ambayo utayaandika katika daftari yako kwa kujifunza kwako kwa baadae. Anza kwa susoma Mwanzo 40.

**ZOEZI**: Sura hii inahusu maofisa wawili waliomtumikia mfalme na sasa wako kifungoni.

- Hawa ni akina na nani na walifanya nini?

  ______________________________________________

- Mwisho wao ni nini? ______________________________________________

  Mkuu wa walizi anawakabidhi kwa nani? ______________________________

- Kulitokea nini kufuatana na mstari wa 5?

  ______________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

- (Mstari wa 6-8) Yusufu anagundua nin asubuhi iliyofuata? ______________________________
  Anawauliza nini? ______________________________________________________
  Jibi lilikuwa lipi? ___________________________________________________________
- Yusufu aliamini kuwa kutafasiri ndoto kulikuwa kwa Mungu. Aliwaambia nini?
  ______________________________________________________
- Mistari 9-11: Ndoto ya mnyweshji likuwani ipi?
- ______________________________________________________
  Tafsiri ya Yusufu ilikuwa ni ipi mistari 12-14?
  ______________________________________________________
- Yusufu alimwomba mnyweshaji kumfanyia nini mistari 14?
  1. ___________________________________
  2. ___________________________________

  Yusufu alimwambia nini mstari 15?
  ______________________________________________________
- Mistari 16-17: Ndoto ya kiongozi wa waokaji ilikuwa nini?
  ________________________________________________________________________________
  tafsiri ya Yusufu ilikuwa ni ipi mistari 18-19? ____________________________________
  ______________________________________________________
- Lilikuwa tukio gani mstari wa 20? ________________________________________________
  Kulitokea nini kwa mnyweshaji mstari 21? _________________________________________
  Kwa mkuu wa waokaji? ______________________________________________________
- Yote yalitokea sawa na Yusufu alivyowaambia katika tafasiri ya ndoto zao. Ni shida gani moja ilikuwa katika mstari wa 23? ____________________________________________

**Somo 3 – Sehemju 2**

**UTANGULIZI**: Kwa mara nyingine inaonekana Yusufu anatendewa isivyo haki. Mnyweshaji wa mfalme amechangamka kutokana na mambo yalliyofahamika siku tatu zilizopita kuwa amemsahau Yusufu na ombi lake la kukumbukwa mbele ya Farao tofauti na alivyoomba. Na mwingine alisahau hata kusema "asamte" amesahau aliyempa habari njema wakati alipokuwa akijisikia hajaliwi. .

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mwanzo , 41:1-40.

**ZOEZI**: Mungu aliwasiliana na watu kupitia ndoto. Tunaona hii kwa mara ya kwanza wakati Yusufu alipokuwa na doto mbili akazishirikisha familia yake katika Mwanzo 37. Tena katika sura ya

40 kiingizi wa wanyweshaji na waokaji kila mmoja alipata ndoto. Miaka miwili baadae ndoto inaleta maana kwa watu wa kipindi hicho katika sehemu ya dunia ya wakati huo. Ndoto ilipotafasiriwa vizuri watu waliamini kuwa ndoto ilikuwa na maana ya maisha ya mtu aliyehusika. Tunapoendelea na mistari hii, inabidi ifahamike kuwa utamaduni wa mashariki ya karibu uliunganisha hali ya hewa, mazao na mahusiano ya ki mungu. Maelezo ya njaa hayakuhusiana na mabadiliko ya hali ya hewa bali ilihusianishwa na Mungu/miungu kukasirikia watu wake.

- Mistari ya 1-4: Nani aliyeota wakati huu? ________________________________________
  Ni ndoto gani? ____________________________________________________
- Farao analala na kuwa na ndoto nyingine. Ni ndoto gani?
  ____________________________________________________
- Farao anafanya nini katika mstari 8?
  ________________________________________________
  Kutafuta wafasiri wa ndoto kulileta matokeo gani? ___________________________

**FUNDISHO**: Mwisho! Mnyweshaji anakumbuka yaliyotokea kwake alipokuwa kifungoni kabla ya kuachiliwa. Anamwambia Farao habari ya kijana wa kiebrania aliyekuwa amefungwa pamoja naye, mtumishi wa mkubwa wa gereza. Fara aliagiza Yusufu aletwe. Anatolewa nje ya gereza, amenyiolewa na kuoshwa vizuri, amebadilishiwa nguo, sasa amesimama mbele yamfalme.

**ZOEZI**: Annza na Mwanzo 41:13.

- Anataka nini toka kwa Yusufu? ________________________________________________
- Yusufu anajibu nini? ____________________________________________________
- Mistari 17-24: Farao anamshirikisha Yusufu ndoto yake. Ni neno gani la mwisho anasema katika mstari wa 24? ____________________________________________________
- Mstari 25: Yusufu anatoa maoni mawili kabla ya kutoa fasiri ya ndoto ya mfalme.
  1. ______________________________________________
  2. ______________________________________________
- Mistari 26-27: Tafasiri ya ndoto yake ni nini? Mungu anatarajia kufanya nini?
  ____________________________________________________
- Yusufu anamwambia farao maana ya ndoto kwa maneno yake. Anasema kuwa Mungu amefunua nini kwa Farao? ______________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

**FUNDISHO**: Mungu anakwenda kuleta miaka saba ya wingi wa chakula juu ya Misri ikifuatwa na miaka saba njaa kali kiasi cha Misri kutokumbuka miaka ya neema. Tunaambiwa katika mstari wa 32 kwamba Mungu alimpa Farao ndoto katika mifumo miwili kwa sababu 1) Mungu alikuwa amekusudia kuenendelea na mpango wake na 2) Angetimiza makusudi yake mapema.

**ZOEZI**: Katika mistari hii inayofuata Mungu anampa Farao maelekezo.

- Yusufu aliwasilisha mpamongo kwa mfalme (mistari 33-36):
    1. Farao alikuwa atazame sifa gani

       ____________________________________________
- Farao na maofisa wake waliitikiaje mpango wa Yusufu? ________________________
  Wasiwasi wao ulikuwa ni nini katika mstari wa 38?

  ___________________________________________
- Uamuzi wa Farao ulikuwa ni nini katika mstari 39?

  _______________________________________

  Ni sifa gani za Yusufu Farao alizoona na kukubali?

  _________________________________________________

  Wajibu wa Yusufu ulikuwa ni upi?

  _____________________________________________

  Nani waliwajibika kwake? __________________________________________________

  Yusufu aliwajibika kwa nani? ______________________________________________

**KUTAFAKARI**: Kijana Yusufu aliyeletwa Misri na kuuzwa kama mtumwa, sasa ni mkubwa wa pili katika Misri. Wote wanaagizwa kuwajibika kwake isipokuwa Farao tu. Unafikirije? Kufuatana na historia ya maisha yake alistahili kupata cheo alichopata? Baraka alizopata mwishoni zilistahili mateso? _______________________________________________________

Inawezekana ni vigumu sana kujifananisha na Yusufu. Labda umedharauliwa kwa kupandishwa cheo. Inawezekana uliona kuwa unastahili kupata nafasi fulani lakini ukadharauliwa. Inawezekana kuwa uliona unastahili kupata kazi fulani badala yake akapewa mtu mwingine ambaye hakuwa na sifa ya kuipata. Inawezekana ulitendewa mabaya sawa na Yusufu alivyotendewa na kaka zake. Inawezekana familia yako ilikudhiaki kama muota ndoto, amabaye hustahili Labda ilionekana kuwa hustahili kuishi na familia ukafukuzwa. Inawezekana ulitendewa kinyume na stahili yako. Inawezekana unalipwa pungufu kufuatana na nafasi yako. Inawezekana hukuthaminiwa kwa wajibu fulani uliofanya . Au ulipuuziwa na rafiki zako katika nafasi ambayo ingeinua maisha yako.

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

Baada ya kujifunza sehemu hii kuhusu maisha ya Yusufu na kuangalia itikio lake katika mazingira tofauti, hatuwezi kusaidia bali hebu tuangalie maitikio yetu katika mazingira na matukio tofauti. Yusufu akiwa mtumishi wa Potifa na msimamizi wa gereza tunaambiwa kuwa Mungu alikuwa pamoja naye. Baraka za Mungu zilikuwa pamoja naye na kufanikisha kwa kila alichokabidhiwa. Kupitia historia ya maisha yake Mungu alimwandaa kwa nafasi Farao aliyompa. Kwanza alikuwa kiongozi katka nyumba na shamba la Potifa. Kisha msimamizi wa gereza alimfanya awe kiongozi wa wafungwa na mambo yote ndani ya gereza. Sasa Yusufu anawajibika kwa maisha yote ya wamisri. Kunung'unika na kulalamika ni jambo linalotokea kwa urahisi. Kutambua mkono na baraka za Mungu kwa yote tunayofanya ni changamoto kubwa. Hii inatualika kwa kiwango kikubwa. Tunaweza kusema, "Inuka juu yake!" Tunaitwa kuwa juu ya matukio yanayotuhusu na kuona na kuamini kwamba Mungu yuko pamoja nasi na kutupatia mafanikio kwa yote tunayoyafanya.

**MATUMIZI BINAFSI**: Tumia muda kutafakari maisha yetu wenyewe. Kumbuka wakati ulipoona kuwa umepuuziwa na kutothaminiwa ipasavyo. Ni mazingira gani unayokumbuka?

_______________________________________________

Matumaini yako yalikuwa ni yapi?

_______________________________________________

Kulitokea nini hasa? _______________________________________________

Itikio lako lilikuwaje kwa hali hiyo? ________________________________________

Ungechagua ifanyikeje tofauti na ilivofanyika? Kwanini?

_______________________________________________

Unapotafakari mazingira yako yaliyopita, unaona inahusianaje na maisha ya sasa?

_______________________________________________

Unapotafakari, ni wapi unaona Mungu yuko pamoja nawe katika mazingira ya sasa? ______________

_______________________________________________

**SALA**: Ee Mungu, ninakiri kuwa mara nyingine huweka juu viwango vya karama na uwezo wangu . Ninaamini kuwa ninastahili nafasi na cheo. Yusufu ni mfano wa uvumilivu. Alitumika kama mtumishi kwa Potifa na msimamizi wa gereza. Asante kwa fursa uliyonipa ya kutumika kama mtumishi na mwajiri, meneja, na nafasi nyingine katika msisha yangu. Yusufu aliishi akiamini kuwa uko kazini ndani yake na kupitia kwake. Nashukuru kwa uwepo wako kwangu sawa na ilivyokuwa kwa Yusufu. Naomba mafanikiao uliyonipa yawe ni njia ya kukutana na maisha ya watu wengine pia.

_______________________________________________

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

**UTANGULIZI**: Farao amemteua Yusufu kuwa mkubwa kwa Misri nzima. Mwanzo 41:41-45 inatwambia kuingizwa kwake ofisini. Tuna sherehe kama hizo mtu anapochaguliwa na usharika kuwatumikia. Kwanza mtu anachaguliwa na kusimikwa. Wakiati huo stola (kwa kawaida nguo ya rangi inapowekwa kwenye shingo ya mchungaji) ikiwakilisha ofisi na wajibu unategemewa kutoka kwa mchungaji. Farao anamteua Yusufu na anamwingiza kwenye wajibu kuonyesha watu wajibu na mategemeo yao kwake.

**KAZI YAKUFANYA**: Soma Mwanzo 41:41-57.

**ZOEZI**:

- Mstari 41: Farao anamwambia nini Yusufu? ________________________________________
- Yusufu alipambwaje kama amiri jeshi mkuu wa pili?
    1. ________________________________________________
    2. ________________________________________________
    3. ________________________________________________
- Mwisho alipandishwa juu ya farasi wa vita! Fikiria mazingira. Msafara ni wa namna gani! Yusufu anapigiwa gwaride na watu Misri kama amiri jeshi mkuu wa pili!
- Farao anajitangaza kama farao na mambo ambayo Yusufu anapaswa kuheshimiwa.
- Anampa Yusufu jina jipya. Ni lipi? __________________________________________
- Farao anampa na mke. Jina lake ni? ___________________________________

**KUTAFAKARI**: Unafikiri Yusufu alistahili haya yote? Do you thin unafikiri hizi sherehe zilizidishwa? Au hapana? Fikiria majukumu makubwa aliyomkabidhi. Ni heshima gani ambayo Farao alitangaza kwa watu? Iliwapasa watu kumpisha njiani; ilibidi wamwinamie Yusufu anapopita sawa na walivyofanya kwa Farao mwenyewe.

Tukikumbuka kuwa Yusufu alikuwa akitumika gerezani muda mfupi uliopita hatuna la kufanya zaidi ya kumtukuza Mungu. Ni yeye aliyemtoa kwenye mauchafu wa gereza na kumweka mahali pa juu.

**KUKARIRI**: Zaburi 40:1-3 inawezekana inaelezea hali ya Yusufu. Labda haya ni maneno ambayo unaweza kujifananisha nayo kwa kushughulika na hali ya maisha yako mwenyewe. Mtunga Zaburi anaongelea juu ya uvumilivu, kadiri anavyomlilia Bwana, akijua kuwuwa anamsikia Yusufu pia alikabiriwa na uchafu wa kisima, safari ya Misri kwa msafara, na gerezani ambako alisahaulika. Siku hii ya kusimikwa kwake ilikuwa ni siku mpya. Bwana anaweka wimbo mpya katika moyo wake, wimbo ambao utawafanya wengine wamtukuze Mungu. Andika mstari huu katika kadi. Hebu wakutumikie

kwa matumaini na furaha. Hebu uwafariji na kuwahakikishia kuwa Mungu yuko pamoja nawe. Hajakusahau wala kukuacha hata kama utafikiri kuwa kushimo jembamba limekudhikilia kama mfungwa wake.

**Domo 3– Sehemu 5**

**ZOEZI**:

- Kutokana mstari wa 46 Yusufu alikuwa na umsri gani alipoanza kutumika kwa Farao? ______
- Elezea miaka ya wingi wa chakula: ________________________________________________
- Mstari 50: Tunaambiwa kuea wakati wa wingi wa chakula Yusufu na walikuwa wapata watoto wawili. (angalia chini notisi za maelezo ya maana zaidi) Majina ya wanawake yalikuwa:
    1. ______________________________, lililomaanisha ____________________________________________
    2. ______________________________, lililomaanixha ____________________________________________
- Ni kwa vipi miaka wa wingi wa chakula unaathiri familia zaidi ya mahitaji ya chakula? Fikiria msongo wa mawazo, maisha ya mafanikio , mwenendo, nk.

  ________________________________________________

  Mwaka mmoja au miwili ya mafanikio inaweza kutuathiri kwa kiasi gani?

  ________________________________________________
- Miaka ya wingi wa chakula ilipoisha miaka ya dhiki ilianza. Tunaambiwa nini juu ya Misri katika mstari wa 54? ________________________________________________

**FUNDISHO**: Wamisri walipoanza kuona athari ya njaa, walikuja kwa Farao ambaye aliwatuma kwa Yusufu ambaye aliwaoelekeza la kufanya. Kadiri njaa ilipoongezeka ghara zilifunguliwa na nafaka ziliuzwa. Pia kulitokea udanganyifu kidogo… Tunaambiwa kuwa nchi zote zilizozunguka ziliathirika kwa njaa, na Misri peke yake ilikuwa na chakula. Hii ilisababisha watu wa nchi zote kuja kununua chakula Misri. "Njaa ilikuwa kubwa dunia nzima."

**KUTAFAKARI**: Ni wakakati wako wa kubashiri. Njaa hii itamleta nani Misri?

________________________________________________

Je Mungu atatumia njaa kurejesha mahusiano yaliyovunjika kati ya watoto na baba? Yakobo na watoto wake hawana chakula huko Canaan wakati Yusufu akitoa msaada wa chakula hukoa Misri.

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

Yusufu amesahau ndugu zake na watu wote wa nyumabani kwa baba yake (mstari 51). Anaamini kuwa ni Bwana aliyemleta Misri kupitia shida alizozipata ili aweze kuwa msaada, katika nchi ambamo alipata mateso.

Katika habari hii tunafahamu zaidi mateso aliyovumilia huko Misri. Hakuongea kimisri alipofika Misri, alikuwa mgeni katika mi;a na desturi za Misri. Alikuwa akifahamika kama mzinzi ambaye alifungwa kwaajili hiyo. Lakini tunaambiwa kuwa Mungu alikuwa pamoja naye. Alipopewa heshima na Farao na kupata watoto tunasikia kilio moyoni mwake miaka yake yote. Kilio chake ni , "Nimefanya nini kustahili haya yote?" Sasa akiwa amiri jeshi wa pili wa nchi, tunasikia kilio chake kilekile, "Nimefanya nini kustahili haya hyote?"

Neema ya Mungu imekuwa na Yusufu miaka yote. Alikuwa akimfahamu Mungu wa Baba zake ambaye alikuwa tofauti na miungu ya Misri. Mungu huyu alikuwa wa huruma kwake. Hakumuacha, hata alipotendewa vibaya. Mungu alitumia uzoefu wake kumtengeneza ili awe mtu anaye mtaka, pasipo yeye kufahamu Mungu alimwandaa ili aungane na baba yake na wote wa nyumbani kwake.

**MATUMIZI BINAFSI**:

- Je uliisha tengana na wale unaowapenda kwa uchungu? Kuna mtu pekee unayemkumbuka?
  ______________________________________________
- Uanaweza ukafikiria ulivyokomaa sasa na kufikiria njia ya kukuwezesha kuungana nao tena?
  ______________________________________________
- NI kwa vipi unaweza kufikiria mateso matatizo yako ya zamani kama jia ya kukufanya ufikirie mambo yajayo? ______________________________________________
- Hali yako ya maisha imebadilikaje tangu kutengana kwako kwa uchungu?
  ______________________________________________

**SALA**: Kwa maneno yako inua kilio chako mbele za Mungu, "Nimefanya nini hata kustahili haya yote?" ___________________________________________________

______________________Na kwa shukrani moyoni mwako kwa uhuru Mungu aliokupatia kwa neema yake katika maisha yako, mwinue Bwana kwa maombi ya shukrani, "Niemefanya nini kustahili haya yote?"

___________________________________________________

Somo 4 Sehemu 1

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

**UTANGULIZI**: Yusufu amefikia kilele cha safari yake. Kwa umri wa miaka kumi na saba alijikuta ndani ya kisima cha maji, kiwa umri wa miaka therathini anajikuta ni amiri jeshi msaidizi wa nchi, ya mafarao. Nchi nayo imefikia lengo. Kwa kipindi cha miaka saba nchi inajikuta ina chakula cha kutosha kiasi cha kujaza maghala. Miaka saba iliyofuata njaa ilisikiwas na kila mtu wa Misri na majirani zake. Kwasababu Farao alimwandaa Yusufu nchi yote ilikuwa imejiandaa vya kutosha kwa janga hili. Habari hii imefahamika. Misri tu ina chakula! Fikiria habari hii ilivyoinufaisha Misri kiuchumi, na kisiasa. ____________________________________________________

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mwanzo 42.

**ZOEZI**: Hali ya chakula Kanaani ni mbaya na Yakobo ana habari kuwa Misri kuna nafaka.

- Katika mistari ya 1na 2 Yakobo inaonekana hawajui cha kufanya na watoto wake. Miaka ishirini imepita tangu ndugu waachane. Ni wakubwa kiasi kwamba ilipasa wawe wanamtunza baba yao mzee. Badala yake unaonaje hali?

  ________________________________________________

  Yakobo anawaambia nini? ____________________________________________

- Mstari wa 3 na 4: Isipokuwa________________________ walisafiri Misri kununua chakula. Kwanini alibaki nyumani?

  ________________________________________________

- Katika mstari 6 inawekwa wazi kuwa Yusufu akiwa ni gavana ndiye aliyesika na kuuza chakula. Ndugu wanafika wanakutana na Yusufu . Kitu gani cha kwanza wanafanya?

  ________________________________________________

- Tunaambiwa nini katika mstari wa 7?

  ________________________________________________

  Yusufu aliwatambua lakina hakuwaambia ila aliwahudumia?

  ________________________________________________

  Aliwauliza nini? ________________________________________________

- Hawa ndugu walikuwa wakitafuta chakula si ndugu yao waliyemmchukia na kumtendea kwa hila na chuki. Pamoja na hayo hali imebadilika. Meza zilibadilishwa. Yusufu alijua kuwa wanatafuta chakula. Angalia mistari ya rejea ukifuatalia neno ndoto mstari 9. Fungua katika rejea na usome habari za ndoto ya Yusufu.
- Yusufu aliendelea kuwatendea kama wageni. Anatoa tuhuma gani kwao katika mstari wa 9?

  ________________________________________________

- Wanaume kumi na Yusufu lakini Yusufu ni gavana. Yusufu alikuwa na nafaka ambazo walipaswa kumpelekea baba yao Kanaani. Yusufu anasisitiza nini? _______

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

________________________________________________

- Mstari wa 13: Wanafunua nini kuhusu familia yao kwa Yusufu?

  ________________________________________________

- Yusufu anakuwa mkali. Anaendelea kuwatuhumu kuwa wapelelezi. Katika mstari wa 15 anaagiza nini? ________________________________________________

  Unafikiri ni kwanini alitoa madai haya? Yusufu anataka kufahamu nini? _________

  ________________________________________________

- Mistari 16-17: Maagizo ya Yusufu yalikua nini?

  ________________________________________________

  Anaendelea kuwatendea kwa ukatili. Alitaka kuhakikisha ukweli wa waliyoyasema. Alitaka kufahamu kama waliyosema kuhusu nyumabani ni kweli.

**Somo 4 – Sehemju 2**

**ZOEZI LINAENDELEA**: Ni siku tatu wakiwa kizuizini.

- Unafikiri hawa ndugu walifikiri na kuongea nini kwa siku hizi? Walikuwa na hisia yoyote ni kwanini huyu mtawala anawatendea kwa ukatili kiasi hiki? Ungekuwa pamoja nao unafikiri ni maongezi gani yalikuwa yakiendelea kati yao?

  ________________________________________________

- Yusufu anabadili amri yake. Wanaume wanaambiwa nini?
  1. Mstari 18: __________________________________________
  2. Mstari 19: __________________________________________
  3. Mstari 20: __________________________________________Mistari 21-22 inaweka wazi maumivu na hisia za hawa ndugu yaliyodumu kwa kipindi hiki chote. Kwa maneno yako elezea hatia waliyobeba kwa kipindi hicho chote?

  ________________________________________________

  Kwanini unafikiri hizo ni fikra zao za kwanza za kutendewa hivyo? Unafikiri ni kwanini walikuwa wakikumbuka miaka 20 iliyopita? _____________________

  Rubeni alitaka kujitakasa. Labda tungemuita "Ndugu niliwaambia". Kulikuwa na lawama gani? ________________________________________________

  Unafikiri hii ilikuwa mara ya kwanza kusema achofanya? __________________________

  Mashitaka yalikuwa ni yapi? ______________________________________________

  Ni fikra gani nzito katika mstari wa 23? Uliisha fikiria hii kabla?

  ________________________________________________

- Yusufu anaitikiaje kwa maongezi ya kaka zake? ___________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Kwa jaziba alipojikusanya tena aliagiza nini?

______________________________________________

- Mstari 25: Yusufu alikuwa mkarimu. Alionyeshaje ukarimu wake?
  1. ________________________________________
  2. ______________________________________na
  3. ________________________________________

**Somo 4 – Sehemu 3**

**KUTAFAKARI**: Yusufu aliwapa ndugu zake wasichostahili. Walitaka kumuua lakini yeye amewaonyesha ukarimu. Rudi kwa Mwanzo 39:21. Yusufu yuko kifungongi. ‚Masta unatueleza kuwa Mungu alikuwa pamoja na Yusufu. Tena unasema kuwa Mungu alimwonyesha huruma na alimpa upendeleo … Fikiria kwa muda mazingira ya Mwanzo 42:25. Tumeona ukarimu wa Yusufu. Sawa na Mungu alivyokuwa naye kwa miaka hiyo yote anaonyesha ukarimu kwa ndugu zake. Inaonekana kuwa Mungu ameweka moyo wa Yusufu kwa ndugu zake. Alifunikwa na upendo akitafuta jinsi ya kupatana nao kwa kuwaonyeha ukarimu.

Tunapaswa kuchua nafasi ya kuangalia itikio la hawa ndugu kwa matendo ya Yusufu ya ukarimu kwao. Inafurahisha kuona kuwa hatia inawasababisha wasipate zawadi ya upendo. Hatia huzuia upendo. Huu ni ukweli unaotuhusu pia. Hatia hututenganisha na nafsi zetu wakati hatuwezi kujisamehe. Hatia hututenganisha na wengine wakati hatuwezi kujisameha kwa yale tunayowatendea wengine. Hatia pia hutufanya kutengana na Mungu. Tuliumbwa na hisia ambayo hutuonya kutokana na dhambi zetu. Tunakuwa na hatia kwa yale tunayomkosea Mungju . Matendo yetu ya dhambi huwa wazi tunapokiri kuwa tumewakosea wengine. Hii hatia tunayoibeba hutufanya tukose vitu vingi lakini maisha ya uhuru yenye uhusiano na Mungu yana baraka nyingi .

Mungu anapenda kutoa upendo wake kwa watu wote. Hii inaitwa neema ya upendo. Neema ya Mungu ni kile ambacho hatuwezi kukipata kwa stahili yetu sawa na upendo wa Yusufu kwa ndugu zake. Yusufu alitaka ndugu zake waanze kufahamu kuwa anawapenda. Aliwasamehe. Mungu anataka tufahamu kuwa hatia tunayoibeba imefunikwa na damu ya Yesu. Yesu ndiye aliyekufa msalabani kwaajili yeutu ili dhambi tulizomkosea ziweze kusamehewa. Tunaamini kuwa uongo unaoendelea kutuambia kuwa bado tuna hatia na kwamba hatuwezi kuwa na upendo wa Mungu Ndiyou ukweli ni kwamba hatustahili upendo wa Mungu; pamoja na hayo mwaliko wa Mungu kwetu ni kupokea zawadi ya upendo wake bure alioutoa kupitia mwana wake Yesu. Andika anayotuambia katika Waefeso 2:8-9. ______________________________________________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Upendo wake ni safi ambao hatustahili kuupata. Ni zawadi ya bure ya Mungu tunayoipata tunapoamini kuwa dhambi zetu zimesamehewa, na hatia yetu imefutwa kupitia kuishi kufa na kufufuka kwa Yesu. Zawadi yake ya msamaha wa dhambi ni uhuru!

**KUKARIRI**: Katika sura hii, Waefeso 2:4, Mtume Paulo anaandika maneno haya: "Kwasababu ya upendo mkubwaa kwetu, Mungu ambaye ni mwingi wa rehema, alitufanya tuishi japo tulikuwa tumekufa kutokana na dhambi zetu—ni kwa neema mmeokolewa." Hiki kifungu kimebeba habari njema za upendo wa Mungu kwetu kupitia Yesu, Weka kifungu hiki kwenye orodha ya kumbikumbu yako. Kila siku upewe nguvu mpya na maneno ya upendo ambao Baba anataka kutushirikisha kadiri tuishivyo kuwa japo si wakamilifu lakini tumesamehewa, tukiwa tumekombolelwa na sasa tuko huru kushirikisha watu wengine upendo wake. .

Somo 4 – Sehemu 4

**MATUMIZI BINAFSI**: Tukikumbuka maisha yetu tunapaswa kuyatazama katika mitazamo ya aina mbili.

- Kwanza kama Yusufu, je kuna mtu aliyenifanyia mabaya? ________________ Nimekumbushwa upendo mkuu wa Mungu kwaajili yangu na jinsi anavyotoa upendo wake kila siku kwaajili yangu. Sasa nataka kuona jinsi ninvyomtendea mtu huyu niliyemtaja jina.
    - Ni kwa vipi maisha yangu yanaonekana katka maisha ya mtu huyu, upendo na wema wa Mungu kwa ukarimu? ________________________________________________ Ni eneo gani la maisha yangu ambalo nataka Mungu awe pamoja nami na kunifanya nifanye mabadiliko ambayo huonyesha wema wake kwa wengine? ________________________________________________
- Tuangalie hatia kwa mtazamo wa ndugu za Yusufu. Je kuna hatika ambayo umeibeba kutokana na maneno uliyoyasema au matendo uliyoyafanya ambayo unayakumbuka moyoni mwako amayo yamesababisha kikwazo kwa mtu fulani? Huyo mtu ni nani? _______ ___________
    - Kilikuwa kikwazo gani? __________________________________________________Si jambo jepesi kwa baadhi yetu kukubali hatia. Sawa na Rubeni; hatukubali makosa badala yake tunayapeleka kwa wengine. Kumbuka hawa ndugu waliobeba hatia kwa kipindi hiki chote. Hawakuamini kama walifanya yale waliyoyafanya. Tunasoma katka Mwanzo 42:21, "Tuliona alivyokuwa na mahangaiko alipotusihi kwaajili ya maisha yake, lakini hatukusikia…" Nafsini mwao wanalia, "Hivi tulifanyaje jambo hlo?"

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

- Tunavyoendelea kukumbuka hatia zetu inabidi tujiulize maswali, "Kwanini nishikilie hatia yangu?" Swali hili linapaswa kujibiwa. Ninaishikilia kwakuwa sijapatanishwa na mtu niliyemkwa? Niko hivyo kwasababu kosa nililolifanya haliwezi kusamehewa? Ninang'ang'ana kwasababu nimezoea na ndivyo ninavoendesha mabo yangu.? Ninajisikia salama kuishi na hatia yangu? Kwanini nang'ang'ana ,nayo? ____________________

  ______________________________________________

- Nitachukua hatua gani juu ya hatia yangu kwasababu najua kuwa hatia si mapenzi ya Mungu? Anataka niishi maisha yaliyo kamili na huru. ________________

  ______________________________________________

**SALA**: Ee, Bwana ninakuja mbele yako na moyo unaosherekea ushindi juu ya hatia. Sina haja ya kubeba hatia ya mambo yaliyopita, nitko tayari kuishi kwa ukamilifu na huru, niwezeshe kuishi hivyo. Kwa imani ninajua kuwa kwa kufa na kufufuka kwa Yesu nimesamehewa. Alikufa kwaajili yangu! Nimewekwa huru niishi nikiongozwa na wewe! Umenionyesha ukarimu wa upendo wako. Niwezeshe kuonyesha ukarimu wa upendo huo kwa watu wengine. Asante kwa kutoshikilia dhambi zangu. Asante kwa kunipenda kwa neema ya upendo wa Yesu Kristo.

_______________________________________________________

## Somo 4 – Sehemu 5

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mwanzo 42: 29-38. Unaweza kufiikiria mazungumzo, au kuyakosa, hawa ndugu wakielekea nyumbani kila mmoja akifikiria swali: "Mungu ametufanyia nini?"

**ZOEZI**: Wana wa Yakobo wamerudi nyumbani. Fikiria hali yao wakisimulia tukio hili kwa baba yao. Fikiria hali ya kitendawili kila mmojawao alichokuwa nacho.

- Mistari ya 30-34 tunaelezwa juu ya taarifa waliyopeleka kwa baba yao. Kila kitu kinasisikia sawa sawa? __________________________________________________
- Katika mstari wa 35 jambo Fulani linatokea. Kumbuka katika mstari wa 27 mmoja wao alipofungua gunia kuwalisha punda wakiwa safarini kwenda nyumbani, akakuta pesa yake imerudishwa ndani ya gunia lake. . Kulitokea nini katika mstari wa 35?

  __________________________________________________

  Walifanya nini walipokuta na hiyo pesa? __________________________________
- Yakobo alishangaa nini kwa watoto wake?

  ____________________________________________

  Vipi kuhusu hili? Unafikiri Yakobo anasema nini kwa watoto wake hawa kumi? ________

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

_____________________________________________________

Katka mstari wa 37 Rubeni anaongea. Alijisikia kuhusika kwa kilichofanyika kwa Yusufu na majonzi ya baba yao. Anasema nini? __________________________________________

- Msimamo wa Yakobo haubadiliki. Itikio lake ni lipi?

  _____________________________________________________

  Yakobo anaweka wazi kuwa upendeleo wake umegeukia kwa Banjamini, mtoto mwingine wa mke wake Raheli.

  Anathibitisha lile lililokuwa kama mapendekezo katka mstari wa 1 kwmba hatambui tena hawa watoto kumi kama watoto wake. .Alitumia maneno gani katika mstari wa 38? _______________________________ Upendeleo wa Yakobo kwa Benjamini unaleta mashaka gani kwa familia?

  _____________________________________________________

**FUNDISHO**: Njaa iliendelea kuwa mbaya katka nchi na Yakobo anagiza tena watoto wake warudi Misri kununua nafaka. Yuda anamwambia baba yao maagizo waliyopewa na serikali ya Misri Yuda alijua kuwa safari yao haitakuwa ya maana iwapo hawatakwenda na Benjamini. Yakobo aliwalalamikia kwanini walitoa habari za Benjamini kwa Gavana wa nchi. Walitoa maelezo kuwa waliulizwa na walisahiriwa, hawakujua kuwa habari hizo zingetukika kinyume na matarajio yao. Yuda alimwapia baba yake kuwa atawajibika kwa Benjamini, na kama baya lolote lingempata angelaumiwa na baba yao maisha yake yote

**ZOEZI**: Shingo upande, Yakobo alikubali Benjamini aende na ndugu zake Misri.

- Fikiria zawadi zote ambazo Yakobo amewapa wanae waende nazo Misri wampelekee mwanamume. Kulikuwa na nini katika mstari wa 12?
- _____________________________________________________

  Yakobo anawaambia ndugu warudishe zile pesa walizorudi nazo kimakosa.
- Ni sala gani ya Yakobo kwa watoto wake kabla ya kuondoka (mstari 14)?

  ______________________

  _____________________________________________________
- Ndugu walikwenda haraka Misri na kuwasili kwa Yusufu na mdogo wao Benjamini. Yusufu anawaagiza nini watumishi wake (mstari 16)?

  _____________________________________________________
- Wanaume walipelekwa nyumbani kwa Yusufu. Mstari wa 18 unatwambia kuwa walikuwa _____________________.
- Kumbuka uharibifu ulioletwa na hatia yao katika mawazo yao. Walimalizaje? ___

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

__________________________________________________

- Waliomba radhi kwa msimamizi wa nyumba ya Yusufu ambaye aliwahakikishia kuwa hakukuwa na tatizo lolote. Wakili anawaambia nini katika mstari wa 23? "Mungu wako, _______________________

  ________________________________________________________________ pesa yako."

**FUNDISHO**: Ukikumbuka , Ni lini ndugu waliachana na Yusufu katika mstari wa 42 na kusafiri kwenda kwa baba yao, pesa waliyopeleka kununulia nafaka waliikuta kwenye gunia (mistari 27, 35). Kumbuka unasoma katika Mwanzo 43:12 kati ya zawadi walizopeleka ni malipo mara mbili ya kulipia na nafaka ya kwanza na watakayonunua.. Unakumbuka kuwa walipofika mra ya pili Yusufu aliwaagiza watumishi wake kuwapeleka nyumbani kwake. Kama ukumbukavyo waliisha tishwa na hofu iliharibu uwezo wao wa kufikiri (mstari 18).

Habari inaendelea ndugu wakimsihi msaidizi wa nyumbabani kwa Yusufu kufuatana na pesa waliyoikuta katika magunia na haja yao ya kutaka kununua nafaka nyingine. Tena inakuja sentesi: "Hatujui ni nani walioweka pesa kwenye mifuko yetu." Wakili anawahakikishia kuwa hawapaswi kiongopa chochote kimsingi alisema, "Sifahamu nani aliweka pesa kwenye magunia yenu maana nilipokea pea zenu. Kumbukumbu zangu zinaonyesha kuwa mliipa pesa zote! Mungu wenu, Mungu wa baba yenu atakuwa ameweka peasa kwenye magunia. Hamnidai chochote." Swali linalopaswa kuulizwa ni "Nani aliyelipia chakula tulichopeleka kama tulikuta pesa kwenye magunia yetu?" Au, "Iwapo pesa zetu zililipia chakula chetu nani alitupatia pesa tulizokuta kwenye magunia yetu?"

Kwa kurudia Mwanzo 42:25 kama tukikumbuka Yusufu aliagiza kila mtu arudishiwe pesa kwenye gunia lake na kupewa masurufu ya njiani. Yusufu alichukua wajibu wa *kulipa madeni yao*. Alilipa madeni ndugu kutoka kwenye akaungi yake mwenyewe. Walikuwa hawana deni walikuwa huru.

**TUNALOJIFUNZA KUTOKA KWA MUNGU**: Kupitia habari hii yote kuhusu Yusufu tumejifunza kuwa Mungu alikuwa pamoja naye alimuonyesha wema na kumpa upendeleo mbele ya watu wengine. Katika mazingira haya ya maisha ya Yusufu na ndugu zake tunajifunza uhusiano ambao Mungu anao pamoja nasi. Japokuwa tumevunja uhusiano wetu nay eye kwa kuchagua kufuata njia zetu wenyewe na kufanya mambo yetu wenyewe pamoja na hayo amechagua kutupa upendo wake mkuu na kutulipia deni la dhambi. Deni lilikuwa ni mauti ya milele na zawadi yake ya upendo ni uzima wa milele kupitia kifo na kufufuka kwa Yesu. Kwa njia hiyo hiyo Yusufu anatuonyesha upendo wa Mungu . Yusufu alilipa deni kwaajili ya ndugu zake . Walimdai kila kitu; akawafanya kutolipa chochote. Alifanya kila kitu, alilipa vyote! Alisamehe deni lao na waliishi huru bila kudaiwa!

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

# MSAMAHA WA MUNGU UHURU WETU

Uliishategemea kuishi bila deni? Uliishaishi maisha huru bila hatia? Huru bila aibu? Huru kutokana na lawamat? Mungu Baba yetu wa mbinguni, anatupatia maisha huru bila deni kwa kupokea imani ya msamaha wa dhambi. .

**ZOEZI LINAENDELEA**:

- Mstari wa 24: Semeoni analetwa kwao. Maandalizi yalifanywa kwaajili ya Gavana kula pamoja nao. Zawadi ziliandaliwa kutolewa. Wanyama walichinjwa na miguu ilioshwa tayari kwa sherehe. Yusufu alikuwa nyumbani kwake kisha ndugu zake wakaja akawapokea. Aliwauliza nini (mstari 27)? ______________________________________________
  Walikuja mbele yake wakasujudu mpaka chini (mstari 28).
- Kisha akauliza kuhusu Benjamini. Miaka mingi imepita. Kwa vyovyote Benjamini alikuwa amebadilika kwahiyo Yusufu alitaka kuhakiki kama ni yeye?

  ____________________________________________

  Unaona kuwa sauti ya ukali iliishaondoka kwenye maneno ya Yusufu alipokuwa akiongea na ndugu zake?
- Mstaeri wa 30 unaonyesha moyo wa Yusufu kwa ndugu zake, hasa kwa Benjamini wa mama yake mwenyewe. Ameshindwa na jaziba anaondoka kutafuta mahali pa kilia. Anakwenda kwenye chumba chake cha faragha na kulia huko. Kile Yusufu alichotoa katka kulia kwake ilikuwa ni msamaha kwa ndugu zake kwa yote waliyomkosea na sasa yuko wazi mbele ya ndugu zake? Ni kwa jinsi gani Yusufu na Benjamini walikuwa karibu kama vijana wadogo? Kutupwa kisimani kuliathiri mahusiano ya hawa ndugu hasa hawa ndugu wawili.

**SALA**: Kwa vyovyote, habari haijaisha. Somo 5 litaendelea na matukio yaliyofuata kati ya Yusufu na ndugu zake. Mungu alivyoendelea kuwa nao na kuwaunganisha, Yuko pamoja nasi akituweka karibu na wale tunao wapenda. Mshirikishe Mungu kile unachotamani kushirikisha wengine ili upendo ule uwafikie wengine ili kuwapa urejesho na maisha pamoja naye milele.

______________________________________________________

### Somo 5 –Sehemu 1

**UTANGULIZI**: Yakobo alikubaliana na Benjamini kwenda na kaka zake Misri. Wakiwa na zawadi nyingi kwaajili ya gavana wa misri pamoja na pesa za kununua nafaka. Hofu iliambatana na hawa wasafiri kwasababu uzoefu wa safari yao ya mwisho haikuwa kama walivyotarajia . Gavana aliongea nao kwa ukali na kuwaweka ndani kwa siku tatu, akidai kuwa mmoja wao abaki kama amana ili kuhakikisha kuwa watakuja na mdogo wao wa mwisho. Na walipofungua mifuko yao walikuta kuwa pesa walizonunulia chakula zilirudishwa. .

 ©2008 FULLVALUE MINISTRIES

Kwa safari hii wanagundua kuwa wameagizwa kwenda nyumani kwa gavana. Walipaswa kula chakula chao cha mchana huko. Kwa hisia zao wanahisi kuwa watakwenda kuwa watumwa ikiwa ni adhabu ya Mungu kwao kutokana na makosa yao ya miaka mingi iliyopita ya kumuuza ndugu yao Yusufu kwa wafanya bishara. Wakili kiongozi anwahakikishia kuwa hawana sababu ya kuogopa chochote. "Hakuna shida msiogope. Mungu wenu, Mungu wa baba zenu amewapa pesa kwenye mifuko yenu." Mwisho ndugu kumi wanaungana na Semeoni aliyeachwa Misri.

Miguu yao ikiwa imeoshwa mifugo yao imelishwa Yusufu anakutana nao mahali pa chakula. Wanamkabidhi zawadi. Kisha anaanza kuwauliza maswali juu ya baba yao na kumuhakikishia kuwa wamemleta mdogo wao wa mwisho Benjamini. Yusufu anashindwa na jaziba alipomuona mdogo wake Benjamini. Anakwenda haraka faraghani kulia. Habari yetu inaishia pale aliporudi chumba cha kulia chakula.

**KAZI YA KUFANYA**: Soma sura yote ya 43.

**ZOEZI**: Baada ta Yusufu kujuweka sawa anarudi na kuagiza chakula kiletwe.

- Fikiria kila mtu ameketi, katika mstari wa 32:
  - Yusufu alilia wapi? ______________________________________________
  - Ndugu walilia wapi? ____________________________________________
  - Wamisri walilia wapi? ___________________________________________

  Kwnini kuna maandalizi ya chakula hiki?

__________________________________________

  Kwanina Yusufu hakukaa na wamisri? Kuna alama gani katika Mwanzo 41:12? ________

  __________________________________________________

- Ni sehemu ipi nyingine tunaambiwa juu ya mpangilio wa kukaa katika mstari wa 33?

  ______________________

  __________________________________________________

  Ni upi mwitikio wa ndugu? ____________________________________________
- Ni lipi linalofurahisha wakati wa kuhudumu chakula? ______________________________

  Walihudumiwa chakula gani? __________________________________________________

  Ni sehemu gani alipewa Benjamini? ___________________________________________

  Inasikika kama wote walipata muda mzuri (mstari 34): "Kwahiyo wali________________na

  _________________________ kwa uhuru."

Somo 5 – Sehemu 2

**KUTAFAKARI**: Hatuwezi kupuuzia kukumbuka mambo muhimu katika ya habari hii katika msistari hii. Kwanini Yusufu hakuwaambia yeye ni nani? Amevutwa zaidi na uwepo wa Benjamini. Ndugu wote kumi na mmoja wako kwenye chumba kimoja. Iko wazi kuwa ameisha wasamehe. Kwanini anawaficha nafsi yske kwa kutojitambulisha kwao?

- Pia kuna jambo la mpangilio wa kukaa. Kwanza kuna maeneo matatu ya kutoa huduma: Kaka zake na Yusufu, na Wamisri,. Tunaambiwa kuwa ilikuwa ni chukizo kwa Wamisri kula na Waebrania. Tunaambia kuwa mpangilio hakukuwa na mpangilio wa meza kuu. Yusufu alikuwa akila peke yake?
- Wamisri walifanikiwaje kujipanga kwa kufuata aliyezaliwa hadi wa mwisho. Wakujuaje? Ndugu walishangaa.
- Je ndugu waligundua kuwa chakula chao kilifanana na cha gavana? Chakula kilichukuliwa toka mezani kwake, sivyo kwa meza ya Wamisri. Je waligundua? Je wote walikuala chakula kinachofanana? Walijali? Jambo hilo lilikuwa la maana kwao?
- Yusufu alimpa mdogo wake Benjamini sehemu kubwa kuliko wengine na tunaambia kuea walikula pamoja na kwa uhuru pamoja naye. Mara zaidi ni sehemu kubwa na bado haonyeshi kujali.

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mwanzo 44.

**ZOEZI**: Habari inaendelea na habari moja zaidi.

- Mistari 1-2: Yusufu anawaagiza nini wasimamizi wa nyumba yake?

  ____________________________

